

A UHURU KATIKA KRISTO. Wagalatia 5:1.

- ❖ Je; Tuko huru katika Kristo dhidi ya nini?
 - Dhidi dhambi (Warumi 6:18)
 - Dhidi hukumu (Warumi 8:1)
 - Dhidi udhalimu wa dunia (Wagalatia 1:4)
 - Dhidi laana ya sheria (Wagalatia 3:13)
 - Dhidi ibada ya sanamu (Wagalatia 4:8)
 - Dhidi utumwa wa sheria (Wagalatia 5:1)
 - Dhidi Ibilisi (Waebrania 2:14)
 - Dhidi mauti ya milele (Waebrania 2:15)
- ❖ wetu wenyewe. Yesu alilipa Gharama hiyo msalabani (1 Wakorontho 6:20; 7:23). Haihitaji sisi kufanya kitu Fulani ili tuwe huru.

B UHURU NA USHUPAVU WA SHERIA. Wagalatia 5:2-12.

- ❖ Kwa nini kukatwa kwa nyama kidogo namna hii ni muhimu kwa Paulo? Ilionekana kama ni kitendo kisicho na maana (Wagalatia 5:2-12)
 - Wale waliokuwa wametahiriwa walikuwa wamejitoa kushika sheria yote ili waokolewe (fg. 3).
 - Huko ni kuhesabiwa haki kwa matendo, hivyo walikuwa wakikataa kuhesabiwa haki aliyoitoa Mungu katika Kristo (fg. 4).
 - Hiki ni kikwazo kikubwa katika ukuaji wa kiroho (fg. 7).
 - Tohara huondoka “kwazo” la msalaba. Unapotaka kujiokoa mwenyewe, injili ya msalaba ni kwazo kwa kiburi cha mwanadamu, maana imetupasa kutambua kuwa tunamtegemea Kristo tu (fg.11).

C SHERIA NA UPOTOVU. Wagalatia 5:13.

- ❖ “Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?” (Warumi 6:2).
- ❖ Badala ya kufurahia dhambi, uhuru wetu hutuongoza kutumika [kuwa watumwa] kwa ajili ya upendo.
- ❖ Ikiwa kwa hiari tutakuwa watumishi [watumwa] kwa sababu tunawapenda majirani zetu, basi twaitimiza sheria (Warumi 13:10).

D FREEDOM AND LAW. Wagalatia 5:14-15.

- ❖ Yesu aliweka wazi: kukariri herufi za sheria na kutimiza kusudi la sheria ni vitu tofauti (Mathayo 5-7).
- ❖ Paulo anatumia neno “kutimiza” kwa sababu humaanisha zaidi ya “kufanya.” Huo utii unasababishwa na Yesu mwenyewe.
- ❖ Sio kukatilia mbali sheria, wala kupunguza sheria na kuwa upendo; ndiyo namna waumini wanaweza kupitia uzoefu wa kusudi na maana ya kweli ya sheria!